TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# MTAALA WA ELIMU CHANGAMANI KWA VIJANA WALIO NJE YA SHULE

IPOSA

**TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA**

# MTAALA WA ELIMU CHANGAMANI KWA VIJANA WALIO NJE YA SHULE

Kimeandaliwa na
Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
S. L. P 20679
Dar es Salaam
**Tanzania 2019**

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, 2019

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuchapa wala kurudufu kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

# DIBAJI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeandaa Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule - MECHAVI. Kwa lugha ya kingereza mpango huu unajulikana kama *"Integrated Programme for Out of School Adolescents - IPOSA.* Mpango huu umezingatia dhima ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya kutoa elimu bora kwa wote, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu wa mwaka 2016. Katika kutekeleza programu hii, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeandaa mtaala, mihutasari, moduli za masomo, miongozo ya kufundishia, upimaji na usimamizi wa MECHAVI. Mtaala huu ni nyenzo ya kuongoza utekelezaji wa MECHAVI ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ikiwa ni miongoni mwa jitihada za serikali za kuwaelimisha vijana na kuwawezesha kujitegemea kwa kuzalisha mali ili kuishi maisha bora. Pia mpango huu unaendeleza utekelezaji wa azma ya serikali ya kutoa elimu kwa vijana kupitia mfumo rasmi na usio rasmi.

Mpango huu wa MECHAVI utatekelezwa na taasisi mbalimbali katika maeneo tofauti nchini Tanzania. Hivyo, ninatoa rai kwa taasisi za serikali na zisizo za serikali zinazotoa elimu kwa vijana walio nje ya shule kushirikiana na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kutumia mtaala huu pamoja na miongozo ya MECHAVI ili kutoa elimu bora kwa vijana.

........................................................

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**Kaimu Kamishna wa Elimu**

## SHUKURANI

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) inapenda kutoa shukurani kwa wadau mbalimbali walioshiriki katika kufanikisha uandishi wa mtaala wa Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule - MECHAVI, mpango unaojulikana pia kama IPOSA. Shukurani ziwaendee Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto – UNICEF kwa kufadhili mpango huu na zoezi la uandaaji wa mtaala huu. Pia, TEWW inathamini juhudi za pamoja za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST) zilizosaidia kukamilisha mchakato wa kutengeneza muhtasari huu. TEWW inaamini kuwa UNICEF na wadau wengine wa elimu wataendelea kufanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya kuwahudumia vijana wa Kitanzania wenye mahitaji anuwai kwa lengo la kuwainua kijamii na kiuchumi. Aidha, TEWW inathamini sana juhudi na mchango walioutoa katika kufanikisha kazi hii kwa manufaa ya watanzania.

Shukurani za pekee ziwaendee wataalamu wafuatao kwa juhudi zao za pamoja katika kukamilisha uandishi wa mtaala huu:

**Waandishi:**

| | |
|---|---|
| Leonia Kassamia | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Simon Magava | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Nana Mbunda | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Baraka Kionywaki | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Dkt Ayubu Kafyulilo | United Nations Children's Fund - UNICEF |
| Placid M. Balige | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Danstan Msamada | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Watougo K. Muganda | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Jackline Mbawala | Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo - SIDO |
| Asanterabi M. Kanza | Vocational Education Training Authority - VETA |
| Leonida Tenga | Taasisi ya Elimu Tanzania |

**Waratibu:**

| | |
|---|---|
| Dkt. Sempeho I. Siafu | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Leonia Kassamia | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |

**Mshauri:**

| | |
|---|---|
| Dkt. Honest Kipasika | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |

**Wahariri:**

| | |
|---|---|
| Johnbosco A. Mihigo | Mhariri mshauri - UNICEF |
| Erick Samba | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |

**Msanifu:**

| | |
|---|---|
| Godlove Kyando | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |

**Wasaidizi:**

| | |
|---|---|
| Zena Rajabu Kazala | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Neema Lumisho | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |

..........................................

**Dkt. Naomi Katunzi**

Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| EWW | Elimu ya Watu Wazima |
| FDC | Folk Development College |
| IPOSA | Integrated Programme for Out of School Adolescents |
| KKK | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| KUK | Kamati ya Usimamizi ya Kitaifa |
| MECHAM | Mpango wa Elimu Changamani Baada ya Msingi |
| MECHAVI | Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule |
| MEMKWA | Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa |
| SIDO | Small Industries Development Organization |
| TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TEWW | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| UNICEF | United Nations International Children's Fund |
| VETA | Vocational Education and Training Authority |
| WEO | Ward Education Officer |
| WEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| NACTE | National Council for Technical Education |

# YALIYOMO


DIBAJI .... iii

SHUKURANI .... iv

VIFUPISHO .... vi

SURA YA KWANZA .... 1

USULI .... 1

1.1 Utangulizi .... 1

1.2 Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (MECHAVI) .... 2

1.3 Matamko ya Kisera .... 2

1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .... 2

1.3.2 Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2015 hadi 2030 .... 3

1.3.3 Dira ya Maendeleo ya Tanzania Hadi Mwaka 2025 .... 3

1.3.4 Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 .... 3

1.4.1 Tamko la Ilani ya CCM .... 4

1.5 Nadharia Zinazounda Mtaala .... 4

1.5.1 Ujenzi wa Umahiri .... 4

1.5.2 Ujifunzaji Huria na Masafa .... 4

1.6 Falsafa ya Elimu .... 4

1.7 Malengo ya Elimu Msingi .... 5

1.8 Shabaha ya Mpango .... 6

1.9 Muktadha wa Mpango .... 6

1.10 Malengo ya MECHAVI .... 6

1.10.1 Lengo Kuu .... 6

1.10.2 Malengo Mahsusi .... 7

SURA YA PILI .... 8

MUUNDO WA MTAALA WA IPOSA .... 8

2.1 Utangulizi .... 8

2.2 Nyanja Kuu .... 8

2.4 Stadi za Maisha ..... 9
2.5 Stadi za Ujasiriamali ..... 9
2.6 Stadi za Kisomo ..... 9
2.7 Umahiri wa Jumla ..... 10
2.8 Umahiri wa Ufundi wa Awali (Sadifu) ..... 10
2.9 Umahiri wa Stadi za Kisomo ..... 13
2.10 Umahiri wa Stadi za Maisha ..... 14
2.11 Umahiri wa Stadi za Ujasiriamali ..... 17
SURA YA TATU ..... 18
MPANGILIO WA MAFUNZO ..... 18
3.1 Utangulizi ..... 18
3.2 Hatua za Mpango ..... 18
3.2.1 Hatua ya Kwanza ..... 18
3.2.2 Hatua ya Pili ..... 18
3.3 Mgawanyo wa Vipindi ..... 19
3.3.1 Hatua ya Kwanza ..... 19
3.3.2 Hatua ya Pili ..... 19
3.4 Walengwa wa MECHAVI ..... 19
3.5 Njia na Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ..... 19
3.5.1 Mafunzo ya Darasani ..... 19
3.5.2 Ujifunzaji Huria na Masafa ..... 20
3.5.3 Mafunzo kwa Vitendo ..... 20
3.5.4 Mafunzo ya Kujishikiza (Uanagenzi) ..... 20
SURA YA NNE ..... 22
UENDESHAJI NA USIMAMIZI ..... 22
4.1 Utangulizi ..... 22
4.2 Rasilimali Watu ..... 22
4.2.1. Walimu ..... 22
4.2.2 Sifa za Walimu ..... 22
4.2.4 Utoaji wa Honoraria ..... 23
4.3 Muundo wa Uendeshaji ..... 24

SURA YA TANO ........ 26

USHIRIKISHWAJI NA UBIA ........ 26

5.1 Utangulizi ........ 26
5.2 Ushiriki wa Wazazi, Walezi na Jamii ........ 26
5.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ........ 26
5.4 Wadau Wakuu ........ 27

SURA YA SITA ........ 28

KUTHIBITI NA KUKUZA UBORA WA MECHAVI ........ 28

6.1 Utangulizi ........ 28
6.2 Mifumo ya Kuthibiti Ubora wa MECHAVI ........ 28
6.3 Viashiria vya Ubora ........ 29
6.3.1 Wawezeshaji / Walimu ........ 29
6.3.2 Zana za Kujifunzia na Kufundishia ........ 29
6.3.3 Kituo cha Kujifunzia ........ 29
6.3.4 Viashiria Vingine ........ 29
6.4 Mifumo ya Ukusanyaji na Utunzaji wa Takwimu ........ 29
6.5 Zana za Ufuatiliaji ........ 30
6.6 Mikakati ya Kukuza Ubora ........ 30
6.6.1 Ngazi ya Taifa ........ 30
6.5.2 Ngazi ya Mkoa ........ 31
6.6.4 Ngazi ya Kata ........ 31
6.6.5 Ngazi ya Kituo ........ 31
6.7 Tathmini ya Matokeo ........ 32
6.8 Hitimisho ........ 32

# SURA YA KWANZA

# USULI

## 1.1 Utangulizi

Juhudi za kupambana na adui ujinga nchini Tanzania zilianza mara tu baada ya kupata uhuru. Tafiti mbalimbali zilizofanyika katika nyakati tofauti, zimekuwa zikibaini uwepo wa makundi ya watoto, vijana na watu wazima ambao hawakufanikiwa kupata ya elimu ya msingi, hivyo kusababisha ongezeko la watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu katika jamii. Ili kukabiliana na ongezeko hilo, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WEST) imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuandaa programu zenye lengo la kutoa fursa kwa watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu ili kupatiwa haki hiyo ya msingi. Baadhi ya programu hizi ni kama zifuatazo:

i. Kisomo chenye manufaa (1970)
ii. Kisomo cha kujiendeleza (1986)
iii. Mtaala mpya uliojikita zaidi kwenye stadi za kazi (1995)
iv. Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA-1995)
v. Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA-1999)
vi. Mpango wa Elimu Changamani Baada ya Msingi (MECHAM-2010)

Mbali na changamoto chache zilizojitokeza katika utekelezaji wake mipango yote hiyo iliendeshwa kwa mafanikio. Kwa mfano, tathmini ya Mpango wa Elimu Changamani Baada ya Msingi (MECHAM) ya mwaka 2016 ilibainisha kwamba ingawa kulikuwa na uhitaji mkubwa kwa walengwa, utekelezaji wa mpango huo uliathiriwa na mdondoko wa udahili wa wanafunzi katika vituo. Mdondoko huo ulisababishwa na mafunzo kuchukua muda mrefu kabla ya kuhitimu, walengwa kushindwa kumudu kuchangia gharama za mafunzo pamoja na kukosekana kwa honoraria kwa wawezeshaji. Changamoto nyingine ni kukosekana kwa vifaa vya kujifunzia kwa fani za ufundi wa awali na pia kutokuwepo kwa walimu wenye sifa za kufundisha fani za ufundi.

Aidha takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya 2012 zilibaini kwamba watoto wenye umri kati ya miaka 14 hadi 17 wapatao 1,500,000 walikuwa nje ya mfumo rasmi wa elimu. Vilevile takwimu za elimu msingi (Basic Education Statistics of Tanzania - BEST) za mwaka 2016 zinaonesha kuwa watoto wenye umri kati ya miaka 14 hadi 17 wapatao 2,256,940 walikuwa nje ya mfumo rasmi wa elimu (hawakuweza kupata elimu kama haki yao ya msingi). Kutokana na taarifa hizo, WEST kupitia TEWW imeona umuhimu wa kuanzisha mpango wa elimu utakaowezesha vijana hawa kupata elimu kama haki yao ya msingi katika mazingira rafiki.

## 1.2 Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (MECHAVI)

Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (Integrated Programme for Out of School Adolescents - IPOSA) ambao umebuniwa kwa kuzingatia kaulimbiu ya *hakuna mtoto anayeachwa* - *"No child is left behind"*. Huu ni mpango unaozingatia mahitaji ya walengwa kama yalivyobainishwa katika tathmini ya mipango ya MEMKWA na MECHAM ukiwa na lengo la kupunguza idadi ya watoto na vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu.

## 1.3 Matamko ya Kisera

Mtaala wa mpango huu umezingatia matamko na sera mbalimbali za kitaifa na kimataifa kwa shabaha ya kutoa fursa ya elimu na mafunzo kwa vijana (wasichana kwa wavulana) walio katika mazingira tofauti. Baadhi ya matamko hayo ni kama:

### 1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua haki ya msingi ya kila mwananchi kupata elimu msingi. Hivyo, mfumo wa elimu unapaswa kuhakikisha kwamba makundi yote ya watu katika jamii, yanapata elimu ya msingi kwa kuweka mazingira wezeshi ya uendeshaji wake.

### 1.3.2 Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2015 hadi 2030

Lengo la 4 linasisitiza kudumisha elimu jumuishi, yenye ubora, inayozingatia usawa na kutoa fursa za ujifunzaji endelevu kwa watu wote. Vilevile, lengo hili linasisitiza uwepo na usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana.

### 1.3.3 Dira ya Maendeleo ya Tanzania Hadi Mwaka 2025

Dira ya maendeleo ya Tanzania inasisitiza utoaji wa elimu bora ili kuwajengea walengwa ubunifu, ugunduzi, maarifa na stadi mbalimbali. Pia inalenga kutoa wataalamu wenye uwezo wa kutatua matatizo ya jamii kwa kutumia sayansi na teknolojia.

### 1.3.4 Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014

Sera ya Elimu na Mafunzo (2014) katika Tamko namba 3.3.1 inatanabahisha kuwa "*Serikali itaendelea kuongeza fursa anuwai za elimu na mafunzo kwa usawa kwa makundi yote ya kijamii katika ngazi zote ikiwemo watoto wenye mahitaji maalum.*"

**Tamko la sera namba 3.3.2** inafafanua kuwa *"Serikali itaondoa vikwazo vinavyozuia fursa ya wanafunzi kuendelea na masomo na kukamilisha mzunguko wa elimu katika ngazi husika" (uk. 42).* Aidha, Sera inasisitiza ushirikiano baina ya serikali na wadau wengine wa elimu kuhakikisha kuwa stadi za mawasiliano, kusoma, kuandika, kuhesabu na ujasiriamali unazingatiwa.

Vile vile katika tamko la sera **namba. 3.3.3** *"Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha kuwa usawa wa kijinsia katika elimu na mafunzo unazingatiwa" (uk. 43).* Sanjari na matamko ya sera, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, Sehemu ya II, na Sehemu ndogo ya A *(5:1,2 na 3),* inafafanua haki za msingi za mtoto ikiwemo haki ya kupata elimu na kutoajiriwa.

**Tamko la Sera namba 3.3.4** linasisitiza juu ya mbinu na muundo wa mafunzo haya; *"Serikali itaweka utaratibu na mazingira wezeshi kuhakikisha elimu na mafunzo ikiwa ni pamoja na elimu ya watu wazima inatolewa kwa ufanisi katika ngazi zote kwa njia mbalimbali ikiwemo Ujifunzaji Huria na Masafa" (uk. 44).*

## 1.4 Tamko la Ilani ya CCM ya mwaka 2015

Tamko la chama tawala linasisitiza kuwa serikali itaendeleza utoaji wa elimu kwa kuwa ni hatua muhimu katika kupambana na changamoto za umasikini na ukosefu wa ajira.

## 1.5 Nadharia Zinazounda Mtaala

Mtaala huu umeandaliwa kwa kuzingatia nadharia na mitazamo mbalimbali kama ifuatavyo.

### 1.5.1 Ujenzi wa Umahiri

Mwelekeo wa ulimwengu unasisitiza kufundisha na kujifunza kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri na mbinu za ufundishaji zinazomfanya mwanafunzi kuwa kiini cha ujifunzaji. Vilevile kupima ujifunzaji kwa namna endelevu kwa kumtaka mwanafunzi kuonyesha uwezo wake wa kutenda kwa viwango vilivyowekwa. Pia ni mwelekeo unaosisitiza mwanafunzi kujipima na kutafakari juu ya kiwango cha umahiri alichoweza kufikia na hivyo kuchochea kujifunza zaidi. Mtaala huu ni mbadala wa mtaala unaosisitiza ujifunzaji maudhui unaosisitiza ujenzi wa maarifa. Umahiri wa kila fani umeoneshwa na unalenga kukidhi mahitaji ya ukuaji wa kijana na mahitaji ya soko la ajira. Msisitizo umewekwa katika kumwezesha mlengwa kujifunza jinsi ya kujitegemea katika maisha yake yote. Walengwa wenye uwezo wa juu wa kutenda na vipaji watapewa fursa ya kuviendeleza katika ngazi mbalimbali na wale wenye vikwazo katika kujifunza watapata usaidizi maalum.

### 1.5.2 Ujifunzaji Huria na Masafa

Msisitizo mwingine ni wa mwanafunzi kujengewa uwezo wa kujifunza kwa kujitegemea kwa kuzingatia mfumo wa Ujifunzaji Huria na Masafa (UHM) na hivyo kuufanya mpango huu kuwa nyumbufu na wenye kuzingatia mahitaji mbalimbali ya walengwa. Mwanafunzi ana uhuru wa kuchagua njia rafiki ya kujifunzia kama vile kuwa darasani muda wote au kujisomea kwa kutumia vitabu (moduli) vyenye maelekezo rafiki ya kujifunzia kwa mfumo wa masafa.

## 1.6 Falsafa ya Elimu

Mtaala huu unazingatia Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea kama inavyoelezwa kwenye Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Falsafa hii imekuwa ndio msingi wa Elimu na Mafunzo Tanzania tangu mwaka 1967. Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea inaweka msisitizo katika mambo yafuatayo:

i. Elimu inayokidhi mahitaji ya jamii au walengwa.
ii. Kukuza vipaji/vipawa na tabia za udadisi.
iii. Kujifunza kwa kuhusisha nadharia na vitendo.
iv. Kukuza kujiamini, kufanya uamuzi na kuthamini utu, na
v. Kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali.

## 1.7 Malengo ya Elimu Msingi

i. Kuwezesha walengwa kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana.
ii. Kuwezesha walengwa kuzingatia misingi ya utawala na sheria.
iii. Kuwezesha walengwa kuthamini utamaduni wa kitanzania na wa jamii nyingine.
iv. Kukuza uwezo wa kufikiri, kubuni na kutatua matatizo.
v. Kuwawezesha walengwa kutambua umuhimu wa maadili, uadilifu na uwajibikaji kama misingi ya raia mwema.
vi. Kuwezesha walengwa kukuza vipaji na kuthamini kazi za sanaa.
vii. Kuwezesha walengwa kuthamini na kupenda kufanya kazi.
viii. Kuwezesha walengwa kutambua, kuthamini na kutumia teknolojia na ufundi.
ix. Kuandaa walengwa kwa ngazi nyingine za elimu na kujifunza kusiko na kikomo.
x. Kuwezesha walengwa kupata fursa ya kujiajiri na/au kuajiriwa.

## 1.8 Shabaha ya Mpango

Mpango huu unakusudia kutatua changamoto mbalimbali kwa vijana lengwa kama ifuatavyo:

i. Kuwa njia mbadala ya kupunguza kasi ya ongezeko la mahitaji ya elimu na ufundi kwa walengwa walio nje ya mfumo rasmi wa elimu.

ii. Kuunga mkono harakati za serikali katika kuelekea uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

iii. Kuandaa vijana watakaoshiriki kikamilifu kutekeleza kwa vitendo kaulimbiu ya "Tanzania ya viwanda."

iv. Kuongeza wigo wa elimu linganifu ya kujiendeleza kwa vijana katika mazingira anuwai.

v. Kuongeza wigo kwa vijana kupata ujuzi na maarifa ya kuweza kuchangia maendeleo binafsi na ya taifa kwa ujumla.

## 1.9 Muktadha wa Mpango

Mpango huu umeandaliwa katika muktadha wa Elimu kwa Wote, na uboreshaji wa upatikanaji wa elimu kwa watoto na vijana waliokosa elimu katika mfumo rasmi. Msisitizo wa Elimu kwa Wote unachochea kuibua mipango mbalimbali ya elimu inayolenga kufikia makundi ya vijana na watu wazima ambao wamekosa fursa ya elimu msingi katika mfumo rasmi. Maendeleo ya sayansi na teknolojia, utandawazi, kaulimbiu ya "Tanzania ya viwanda" na dira ya Tanzania kuelekea uchumi wa kati vinachagiza vijana wawezeshwe ili kukabiliana na mabadiliko endelevu kwa kuzingatia usawa wa mahitaji ya mazingira na rasilimali zinazowazunguka.

## 1.10 Malengo ya MECHAVI

### 1.10.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la mpango huu ni kuwa na vijana wenye maarifa, ujuzi, stadi na mwelekeo wa kujitegemea na kuweza kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya jamii inayowazunguka na taifa kwa ujumla.

### 1.10.2 Malengo Mahsusi

Baada ya kuhitimu mafunzo ya mpango huu mlengwa awe na uwezo wa:

i. Kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ili zimwezeshe kupata maarifa na ujuzi wa ufundi.

ii. Kujitambua, kuhimili mihemko na msongo wa mawazo, kujenga na kulinda afya bora, kuwa mbunifu, kuongoza, kujiajiri na kuajiriwa, kuhudumia jamii, kuheshimu jinsia na kutunza mazingira.

iii. Kumudu stadi za ufundi wa awali na ujasiriamali zitakazomwezesha kukabiliana na maisha yake na jamii inayomzunguka.

# SURA YA PILI

# MUUNDO WA MTAALA WA IPOSA

## 2.1 Utangulizi

Mtaala huu wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule umeandaliwa kwa kuzingatia nadharia za ujenzi wa maana (*constructivism*) ili kujenga umahiri kwa walengwa wa mpango. Sehemu hii inaelezea muundo wa mpango huo.

## 2.2 Nyanja Kuu

Mtaala huu una nyanja nne za kujifunza ambazo ni stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, ufundi wa awali, stadi za ujasiriamali na stadi za maisha.

## 2.3 Stadi za Ufundi wa Awali (Sadifu)

Ufundi wa awali ni stadi ambazo zinawawezesha walengwa kujifunza fani mbalimbali zitakazowawezesha kujiajiri katika mazingira yao. Hii inatokana na mahitaji yaliyoibuliwa katika utafiti mdogo wa kutambua mahitaji ya kielimu ya watoto na vijana walio nje ya shule. Hata hivyo, walengwa wataweza kupata stadi za msingi za ufundi zitakazowawezesha kuzalisha bidhaa zinazokubalika katika mazingira yao. Kwa kuanzia fani hizo zinahusisha maeneo yafuatayo:

i. Usindikaji wa vyakula na vinywaji.

ii. Kufunga umeme wa majumbani.

iii. Ufuaji na uhunzi wa vyuma/ufundi chuma.

iv. Kilimo cha bustani.

v. Ufugaji.

vi. Ushonaji, ufumaji na utengenezaji wa batiki na vikoi.

vii. Useremala.

viii. Uashi.

ix. Utengenezaji wa sabuni, mafuta na mishumaa.

## 2.4 Stadi za Maisha

Nyanja hii ya stadi maisha inahusisha maarifa na stadi za kumwezesha mlengwa kujitambua, kuyafahamu, kuyatafsiri na kuyakabili mazingira yake kwa maendeleo endelevu. Inahusisha maeneo tisa ya kujifunzia kama ifuatavyo:

i. Makuzi ya binadamu.
ii. Mihemko na msongo wa mawazo.
iii. Elimu ya afya ya uzazi.
iv. Jinsia na umuhimu wa kufanya kazi.
v. Kutunza mazingira.
vi. Kuepuka dawa za kulevya.
vii. Kuwa mbunifu.
viii. Kujenga uwezo wa kuongoza.
ix. Kuhudumia jamii.

## 2.5 Stadi za Ujasiriamali

Mtaala huu unaweka kipaumbele katika stadi za ujasiriamali ili kumwezesha mlengwa kutumia fursa zilizopo kuanzisha na kuendeleza miradi kwa maendeleo endelevu. Ni matarajio kuwa walengwa wataweza kumiliki biashara na hivyo kuinua hali zao za maisha kwa kuinua kipato binafsi na familia. Stadi hizo zinahusisha maeneo yafuatayo:

i. Dhana ya ujasiriamali.
ii. Kupanga biashara.
iii. Kufanya biashara kwa maendeleo endelevu.

## 2.6 Stadi za Kisomo

Stadi za kisomo zinatambulika na jamii za kimataifa kuwa ni msingi wa maendeleo katika jamii. Mtaala huu unasisitiza ujenzi wa stadi hizi ili kuwawezesha walengwa wasiokuwa na stadi hizo kuzipata kama haki yao ya msingi ili wazitumie katika shughuli zao za kila siku. Stadi hizo ni kama zifuatazo:

i. Kusoma.
ii. Kuandika.
iii. Kuhesabu.
iv. Kuwasiliana.

## 2.7 Umahiri wa Jumla

Walengwa katika mpango wa elimu changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu wataweza:

i. Kutumia maarifa na stadi za ufundi kuanzisha miradi na kujiongezea kipato.

ii. Kujitambua na kuchukua hatua katika kuzikabili changamoto za maisha katika mazingira wanayoishi.

## 2.8 Umahiri wa Ufundi wa Awali (Sadifu)

**Jedwali 2.1: Umahiri wa Ufundi wa Awali (Sadifu)**

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | Umahiri mahsusi |
|---|---|---|
| Ufundi wa awali | Kusindika vyakula na vinywaji | i. Kuchagua teknolojia na mazingira.<br>ii. Kutambua njia za kufungasha bidhaa.<br>iii. Kubaini mfumo wa utambuzi wa majanga na hatua kuu za udhibiti (HACCP).<br>iv. Kuainisha taratibu mbalimbali za usindikaji na biashara ya vyakula.<br>v. Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji.<br>vi. Kufanya mazoezi kwa vitendo.<br>vii. Kubaini masuala ya mazingira na rasilimali za nishati zinazohusika na sekta ya usindikaji vyakula. |

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | Umahiri mahsusi |
|---|---|---|
| | Kufunga umeme wa majumbani | i. Kuzingatia usalama wa karakana, vifaa, zana na mazingira ya kazi.<br>ii. Kutunza vifaa, zana na nyenzo za kazi.<br>iii. Kufanya ukarabatikinga.<br>iv. Kuzingatia maandalizi ya vifaa-kazi mezani (benchworks).<br>v. Kufunga na kuunga mzunguko wa saketi rahisi.<br>vi. Kuchora na kufunga saketi ya taa.<br>vii. Kutandaza mabomba ya nyaya za umeme.<br>viii. Kufunga swichi na vifaa kinga.<br>ix. Kuimarisha usalama, ukarafati na ukarabati wa mfumo. |
| | Kufua vyuma | i. Kuhakikisha usalama katika banda la uhunzi.<br>ii. Kuainisha chuma na kazi zake.<br>iii. Kuchoma chuma na teknolojia yake.<br>iv. Kuunda bidhaa.<br>v. Kuhakikisha ubora wa chuma |
| | Kulima bustani | i. Kuandaa mahitaji ya kilimo cha bustani.<br>ii. Kulima na kutunza bustani kwa kutumia mbinu za kisasa.<br>iii. Kuvuna na kuhifadhi mazao ya bustani |
| | Kufuga kuku, samaki na Nyuki | i. Kubaini sifa na umuhimu wa ufugaji wa kisasa wa kuku, samaki na nyuki.<br>ii. Kutambua mahitaji ya ufugaji wa kisasa wa kuku, samaki na nyuki.<br>iii. Kuzalisha vifaranga vya kuku na samaki.<br>iv. Kufuga kuku, samaki na nyuki.<br>v. Kuvuna na kuhifadhi mazao ya kuku, samaki na nyuki. |

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | Umahiri mahsusi |
|---|---|---|
| | Kushona na kufuma | i. Kuzingatia usalama wa karakana, vifaa, zana na mazingira ya kazi.<br>ii. Kutunza vifaa, zana na nyenzo za kazi.<br>iii. Kutumia stadi za msingi za kushona.<br>iv. Kupima, kukata na kushona nguo rahisi.<br>v. Kudarizi.<br>vi. Kupachika maua / mapambo kwenye nguo. |
| | Kutengeneza batiki | i. Kuandaa malighafi na vifaa vya kutengeneza batiki.<br>ii. Kutengeneza batiki kwa mafundo, mishumaa na kuchovya.<br>iii. Kuzingatia usalama wa vifaa, dawa na mazingira.<br>iv. Kufungasha na kuuza bidhaa za batiki. |
| | Kutengeneza samani mbalimbali (useremala) | i. Kuzingatia usalama wa karakana, vifaa, zana na mazingira ya kazi.<br>ii. Kutunza vifaa, zana na nyenzo za kazi.<br>iii. Kuandaa mbao.<br>iv. Kutumia stadi za msingi za useremala.<br>v. Kutengeneza samani.<br>vi. Kutengeneza viambaza / kingo za milango na madirisha.<br>vii. Kupaua na kuezeka.<br>viii. Kujenga majukwaa na kwego (ngazi).<br>ix. Kutengeneza milango na madirisha.<br>x. Kupachika milango na madirisha. |
| | Kujenga majengo (uashi) | i. Kuzingatia usalama wa karakana, vifaa, zana na mazingira ya kazi.<br>ii. Kutunza vifaa, zana na nyenzo za kazi.<br>iii. Kufyatua tofali za aina mbalimbali.<br>iv. Kujenga msingi na ukuta.<br>v. Kukamilisha ukuta na sakafu.<br>vi. Kusimika madirisha na milango.<br>vii. Kujenga mfumo wa maji safi na maji taka.<br>viii. Kupaua na kuezeka nyumba.<br>ix. Kupaka rangi |

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | Umahiri mahsusi |
|---|---|---|
| | Kutengeneza sabuni, mafuta na mishumaa | i. Kutambua aina za sabuni, mafuta na mishumaa na matumizi yake.<br>ii. Kuchagua teknolojia na malighafi kulingana na mahitaji.<br>iii. Kuandaa mahitaji na vifaa vya kutengeza sabuni, mishumaa na mafuta.<br>iv. Kutengeneza sabuni, mishumaa na mafuta kwa kufuata hatua sahihi.<br>v. Kufungasha sabuni, mishumaa na mafuta. |

## 2.9 Umahiri wa Stadi za Kisomo

**Jedwali 2.2: Umahiri wa Stadi za Kisomo**

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | Umahiri mahsusi |
|---|---|---|
| Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu | Kusoma | i. Kusoma maneno, sentensi na kifungu cha habari.<br>ii. Kusoma kwa kuzingatia alama za maneno kama vile nukta, mkato, kiulizi, n.k.<br>iii. Kubaini fasili na maana za maneno.<br>iv. Kujenga matamshi sahihi ya maneno.<br>v. Kufasili, kutafsiri na kudadisi. |
| | Kuandika | i. Kuunda maneno, sentensi na habari (kwa kutumia alfabeti).<br>ii. Kuandika kwa kuzingatia alama za maneno.<br>iii. Kuainisha makundi ya maneno. |
| | Kuhesabu | i. Kuhesabu namba / numerali.<br>ii. Kutumia matendo ya hesabu (+, -, ÷, x) na kumudu hesabu za ankara.<br>iii. Kumudu elimuumbo rahisi.<br>iv. Kubaini na kutumia vipimo mbalimbali kama vile ujazo, eneo, uzito, urefu, kimo.<br>v. Kukusanya takwimu na kuzitumia. |
| | Kuwasiliana | i. Kusikiliza na kuelewa.<br>ii. Kujieleza kwa ufasaha.<br>iii. Kutumia stadi za mawasiliano. |

## 2.10 Umahiri wa Stadi za Maisha

**Jedwali 2.3: Umahiri wa Stadi za Maisha**

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | Umahiri Mahsusi |
|---|---|---|
| Stadi za maisha | Kuwa mbunifu | i. Kueleza dhana ya ubunifu.<br>ii. Kufafanua vichocheo vya ubunifu.<br>iii. Kubainisha hatua za kufuata katika kubuni.<br>iv. Kueleza faida za ubunifu.<br>v. Kukabiliana na changamoto za ubunifu. |
| | Kujenga uwezo wa kuongoza | i. Kueleza dhana ya uongozi.<br>ii. Kubaini mbinu bora za kuongoza.<br>iii. Kufanya maamuzi sahihi.<br>iv. Kukabiliana na hali ya kushindwa. |
| | Kujiajiri na kuajiriwa | i. Kueleza dhana ya ajira, aina za ajira, na namna ya kuchagua kazi.<br>ii. Kufafanua sifa za kuanzisha au kujiunga na kazi.<br>iii. Kueleza namna ya kutafuta eneo na watu wa kufanya nao kazi. |
| | Kufanikiwa katika kazi | i. Kuandaa na kuzingatia mpango kazi.<br>ii. Kujenga mahusiano mema kazini.<br>iii. Kutumia muda na fedha kwa ufanisi. |
| | Kushiriki kutoa huduma za kijamii | i. Kufafanua dhana ya huduma za kijamii.<br>ii. Kutoa msaada kwa siri.<br>iii. Kujitolea kufanya huduma za kijamii. |
| | Kutekeleza mradi wa kuhudumia jamii | i. Kubainisha mahitaji ya jamii.<br>ii. Kuchagua mradi wa kuhudumia jamii.<br>iii. Kupanga mradi wa kuhudumia jamii.<br>iv. Kutekeleza mradi wa kuhudumia jamii.<br>v. Kukamilisha mradi wa kuhudumia jamii. |

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | Umahiri Mahsusi |
|---|---|---|
| | Kujenga stadi za kujitambua | i. Kufafanua dhana ya kujitambua.<br>ii. Kutambua vipaji ulivyonavyo na jinsi ya kuviendeleza.<br>iii. Kufafanua dhana ya mabadiliko ya mwili.<br>iv. Kutambua haki na wajibu wa vijana katika jamii. |
| | Kukabiliana na mihemko na msongo wa mawazo | i. Kufafanua dhana ya mhemko na msongo wa mawazo.<br>ii. Kubainisha makundi yanayoathirika zaidi na msongo wa mawazo.<br>iii. Kubainisha njia za kumudu msongo wa mawazo.<br>iv. Kueleza namna ya kukabiliana na migogoro. |
| | Kuwa na afya bora ya uzazi | i. Kufafanua dhana ya afya bora ya uzazi.<br>ii. Kubainisha via vya uzazi na matumizi yake.<br>iii. Kubainisha via vya uzazi vya ndani na nje vya mwanamke na mwanaume.<br>iv. Kutumia njia za kupanga uzazi. |
| | Kujikinga na magojwa ya ngono, virusi vya ukimwi (VVU) na ukimwi | i. Kueleza dhana ya magonjwa ya ngono, virusi Vya UKIMWI na UKIMWI.<br>ii. Kuainisha magonjwa, dalili na athari zake.<br>iii. Kufafanua uhusiano kati ya magonjwa ya zinaa na UKIMWI.<br>iv. Kueleza namna nya kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI.<br>v. Kubainisha haki na wajibu katika masuala ya VVU na UKIMWI.<br>vi. Kueleza madhara ya kutopima VVU. |

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | *Umahiri Mahsusi* |
|---|---|---|
| | Kuheshimu jinsia | i. Kufafanua dhana ya jinsi na jinsia.<br>ii. Kuainisha mgawanyo wa kazi kijinsia.<br>iii. Kukabiliana na ukatili wa kijinsia.<br>iv. Kueleza dhana potofu kuhusu jinsi na jinsia.<br>v. Kueleza dhana ya ukatili wa kijinsia.<br>vi. Kuchukua hatua za kukabiliana na ukatili wa kijinsia. |
| | Kukabiliana na uharibifu wa mazingira. | i. Kufafanua dhana ya kutunza mazingira.<br>ii. Kueleza vyanzo vya uharibifu wa mazingira.<br>iii. Kufafanua namna bora ya kutunza mazingira. |
| | Kuzingatia kanuni bora za mtindo wa maisha | i. Kufafanua dhana ya usafi binafsi.<br>ii. Kueleza dalili za mtu anayetumia dawa za kulevya.<br>iii. Kufafanua sababu za vijana kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya.<br>iv. Kufafanua athari za matumizi ya dawa za kulevya.<br>v. Kubainisha njia za kuepuka matumizi ya dawa za kulevya. |

## 2.11 Umahiri wa Stadi za Ujasiriamali

**Jedwali 2.4: Umahiri wa Stadi za Ujasiriamali**

| Eneo la ujifunzaji | Umahiri wa jumla | Umahiri Mahsusi |
|---|---|---|
| Ujasiriamali | Kufafanua umuhimu wa ujasiriamali | i. Kufafanua dhana muhimu za ujasiriamali (ujasiriamali, mjasiriamali, sifa za mjasiriamali).<br>ii. Kubaini masuala muhimu katika ujasiriamali (kutathmini na kukabiliana na hatari katika biashara). |
| | Kuandaa mpango wa biashara | i. Kuainisha fursa zilizopo za biashara na kuweka kipaumbele.<br>ii. Kufanya maamuzi sahihi.<br>iii. Kuanzisha biashara (wazo la biashara, mpango wa biashara, andiko mradi, kubaini vyanzo vya fedha na mitaji, na mikopo). |
| | Kufanya biashara kwa maendeleo endelevu | i. Kuendeleza biashara (kusajili biashara, kutafuta masoko - *4P - market mix*).<br>ii. Kutunza kumbukumbu za biashara (umuhimu wa kutunza kumbukumbu, aina ya kumbukumbu, njia za kutunza kumbukumbu, kukokotoa gharama na kupanga bei, hesabu za faida na hasara, umuhimu wa kutoa na kupata stakabadhi).<br>iii. Kuanzisha na kuendeleza vikundi vya ujasiriamali.<br>iv. Kuzingatia kanuni za mahusiano kati ya familia na biashara (dhana ya familia, mazingira yanayozunguka biashara, mahusiano kati ya familia na biashara, mahusiano kati ya biashara na taasisi husika). |

# SURA YA TATU

# MPANGILIO WA MAFUNZO

## 3.1 Utangulizi

Mpangilio wa programu hii unahusisha hatua za ujifunzaji, mgawanyo wa vipindi, njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia na zana za ujifunzaji.

## 3.2 Hatua za Mpango

Programu hii itakuwa na hatua mbili za ujifunzaji ambazo ni hatua ya kwanza na hatua ya pili.

### 3.2.1 Hatua ya Kwanza

Hatua hii itawahusu walengwa wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Hatua hii ina lengo la kujenga umahiri katika kusoma na kuandika kifungu cha habari kwa ufasaha na pia kutumia matendo ya kujumlisha na kutoa tarakimu zisizozidi mbili. Katika hatua hii mlengwa atajifunza utangulizi wa stadi za maisha, stadi za ujasiriamali na fani moja ya ufundi wa awali atakayoichagua. Hatua hii itachukua kipindi cha miezi 3 hadi 5. Mwishoni mwa hatua hii mlengwa atafanyiwa tathmini ili kuendelea na hatua inayofuata.

### 3.2.2 Hatua ya Pili

Hatua hii imeandaliwa maalumu kwa ajili ya vijana waliohitimu hatua ya kwanza na kwa wale ambao walipitia mfumo rasmi na wana stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu. Katika hatua hii walengwa wataendeleza maarifa ya stadi za kisomo walizojifunza katika hatua ya kwanza, na kuendelea na stadi za ufundi wa awali, stadi za ujasiriamali na stadi za maisha. Hatua hii itatolewa kwa kipindi cha miezi 12 hadi 15. Hii ni hatua ya mwisho katika programu ya MECHAVI ambapo mwanafunzi aliyefikia hatua hii atafanya mtihani wa mwisho na kupewa cheti kulingana na ufaulu wake.

### 3.3 Mgawanyo wa Vipindi

Vipindi vya ujifunzaji vimegawanyika katika hatua kuu mbili.

#### 3.3.1 Hatua ya Kwanza

Katika hatua hii, mgawanyo wa vipindi vya KKK utakuwa 40%, Ufundi wa Awali utakuwa 20%, Stadi za Maisha utakuwa 20% na Ujasiriamali utakuwa 20%.

#### 3.3.2 Hatua ya Pili

Katika hatua hii, mgawanyo wa vipindi vya Ufundi wa awali utakuwa 40%, KKK utakuwa 20%, Stadi za Maisha utakuwa 20% na Ujasiriamali utakuwa 20%.

### 3.4 Walengwa wa MECHAVI

Mpango huu unalenga makundi mbalimbali wakiwemo:

i. Vijana wenye umri wa miaka 14+ ambao hawakupata fursa ya kujiunga na shule ya msingi kwa sababu mbalimbali zikiwemo; umaskini, ulemavu, yatima, umbali wa kutoka shule, mazingira yasiyo rafiki ya utoaji wa elimu, ajira za watoto, kupitiliza umri, mimba na ndoa za utotoni, jamii kutokuthamini elimu, miundombinu isiyokidhi mahitaji ya wanafunzi shuleni, kukosekana kwa chakula shuleni, usalama mdogo shuleni, na nyinginezo.

ii. Vijana walio na umri wa miaka 14+ ambao wameacha elimu ya shule ya msingi kutokana na sababu mbalimbali.

iii. Wahitimu wa darasa la saba ambao hawakupata nafasi ya kuendelea na kidato cha kwanza.

iv. Wahitimu wa MEMKWA.

v. Vijana walioshindwa kuendelea na masomo katika vyuo vya VETA na FDCs.

### 3.5 Njia na Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Elimu katika mpango huu, itatolewa kwa njia zifuatazo:

#### 3.5.1 Mafunzo ya Darasani

Mafunzo haya yatatolewa kwa vipindi vya ana kwa ana kwa muda wa

saa 4 kwa siku. Mafunzo haya yatatolewa muda wa asubuhi au jioni kutegemeana na nafasi ya walimu na upatikanaji wa vyumba vya kufundishia.

### 3.5.2 Ujifunzaji Huria na Masafa

Mbinu hii itatumika kwa baadhi ya fani kutegemeana na mahitaji. Wanafunzi watapatiwa moduli za kujifunzia zitakazomsaidia mwanafunzi kujifunza akiwa peke yake. Aidha, mwanafunzi atalazimika kukutana na mwalimu wake kwa kadiri itakavyoratibiwa. Ili kurahisisha zoezi zima la ufundishaji na Ujifunzaji kwa Njia ya UHM, miongozo maalum kwa wanafunzi na walimu inayozingatia nadharia ya UHM itaandaliwa.

### 3.5.3 Mafunzo kwa Vitendo

Programu hii itahusisha mafunzo kwa vitendo ili kujenga umahiri uliokusudiwa katika kila nyanja. Mafunzo haya yatafanyikia katika vituo vya kujifunzia vyenye vifaa vinavyohitajika.

### 3.5.4 Mafunzo ya Kujishikiza (Uanagenzi)

Wanafunzi wa mpango huu watashikizwa katika asasi/taasisi inayoshughulika na uzalishaji au utoaji huduma kulingana na fani wanayojifunza. Huko watapata fursa ya kukutana na wataalamu na hivyo kujifunza kwa vitendo shughuli mbalimbali kutegemeana na fani zao. Mafunzo haya yatachukua muda wa mwezi 1 hadi 3 kutegemeana na aina ya fani anayosoma mwanafunzi.

## 3.6 Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Katika mpango huu kutakuwa na zana mbalimbali za kujifunzia na kufundishia. Uandaaji wa zana hizo utazingatia maeneo makuu 4 ya ujifunzaji ambayo ni: stadi za kisomo, stadi za ufundi wa awali, stadi za ujasiriamali na stadi za maisha. Kutakuwa pia na vitabu vya mwanafunzi (moduli) vitakavyomsaidia mlengwa kujifunza kwa kila hatua kulingana na uwezo wake. Vitabu hivi vitaandaliwa na TEWW kwa kuzingatia nadharia za ujenzi wa umahiri na pia ujifunzaji huria na masafa unaomfanya mwanafunzi kuwa kiini

cha ujifunzaji wake. Vilevile, mpango huu unasisitiza matumizi ya zana zinazopatikana katika mazingira husika ya walengwa ikiwa ni pamoja na vituo vya ufundi vitakavyobainishwa kusaidia utoaji wa mafunzo haya. Zana hizo ni za ufundi wa awali kwa fani ambazo ni kipaumbele kwa wakati wa sasa ili kusaidia taifa kuweza kufikia uchumi wa viwanda. Aidha zana za stadi za KKK zitaandaliwa kuzingatia hatua za ujifunzaji katika maeneo ya stadi za maisha, stadi za ujasiriamali na stadi za ufundi wa awali. Katika kila eneo la ujifunzaji kutakuwa na miongozo ya kufundishia itakayomsaidia mwalimu kufanya kazi yake kwa ufanisi. Aidha, katika mpango huu kutakuwepo na zana/vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa ajili ya walengwa wenye mahitaji maalumu.

## SURA YA NNE

## UENDESHAJI NA USIMAMIZI

### 4.1 Utangulizi

Ili kuhakikisha kwamba MECHAVI inawafikia walengwa kama ilivyokusudiwa, kutahitajika kuwepo na rasilimali watu, vifaa na mifumo sahihi ya uendeshaji na usimamizi. Hivyo TEWW kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST), pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itasimamia mpango huu kwa kuweka mifumo ya uendeshaji yenye tija. Vilevile, itahakikisha inafuatilia utekelezaji ambao kwa kiasi kikubwa utafanyika katika vituo vilivyo kwenye halmashauri husika.

### 4.2 Rasilimali Watu

Sehemu kubwa ya utekelezaji itafanywa na walimu.

#### 4.2.1. Walimu

Katika utekelezaji wa mpango, MECHAVI itatumia walimu wa shule za msingi wenye ajira rasmi ya Serikali. Walimu hao watakaobainishwa na TEWW kwa kushirikiana na halmashauri husika, watapatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika nyanja mbalimbali kama zinavyoonekana katika mtaala wa MECHAVI. Aidha, katika kila eneo la ujifunzaji watachaguliwa angalau walimu watatu kutoka kila shule/ taasisi zitakazobainishwa kuendesha mpango huu. Utaratibu maalum utawekwa kwa ajili ya kuwatambua walimu wenye uelewa mzuri juu ya uendeshaji wa mpango huu.

#### 4.2.2 Sifa za Walimu

Idhibati ya uwezeshaji wa MECHAVI itatolewa na TEWW kwa kushirikiana na wadau wa utoaji mafunzo kwa walimu watakaobainishwa kuwa na sifa stahiki. Sifa za walimu watakakaobainishwa ni kama ifuatavyo:

i. Ujuzi na maarifa katika eneno husika.

ii. Uwezo wa kuhamasisha wanafunzi kujifunza ipasavyo.

iii. Mahusiano mazuri na wanafunzi.
iv. Uwezo wa kuandaa zana kwa kutumia rasilimali zilizopo katika mazingira.
v. Uwezo wa kuwasilisha maendeleo ya wanafunzi kwa wakati.
vi. Uwezo wa kumsaidia mwanafunzi kutumia maarifa na ujuzi alioupata katika kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi.
vii. Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuwezesha somo lake.
viii. Uwezo wa kuleta matokeo bora kwa wanafunzi.
ix. Uwezo wa kutumia mbinu shirikishi katika ujifunzaji.
x. Uwezo wa kufundisha kwa kuzingatia mila na desturi za eneo husika.

### 4.2.3 Rasilimali Vitu

Mpango huu utatumia miundombinu iliyopo kutolea mafunzo kama majengo ya umma yaliyopo kwenye jamii kama vile shule za msingi, vyuo vya ufundi, shule za sekondari, vyuo na taasisi mbalimbali za umma kulingana na sheria ya elimu Na. 30. Hata hivyo, ili kuleta ufanisi, TEWW itafanya tathmini ya kubaini vituo vyenye rasilimali zitakazowezesha mpango huu kuendeshwa kwa urahisi. Rasilimali zitakazotumika kama kigezo cha kuidhinisha kituo cha MECHAVI zitajumuisha: zana za kujifunzia na kufundishia, vifaa za kujifunzia na kufundishia, samani, majengo, mahali kituo kilipo, nafasi/eneo linalotosha kuendesha mafunzo, uwepo wa umeme na maji n.k kama itakavyoainishwa katika miongozo itakayotolewa.

### 4.2.4 Utoaji wa Honoraria

Kutokana na miongozo ya uendeshaji wa EWW nchini, walimu wa madarasa ya kisomo wanatakiwa kupata honoraria kwa kazi ya kufundisha wanayoifanya katika ngazi ya kituo. Hii inatokana na kuwa, haki ya kupata elimu, hususani ya msingi ni ya kila mtanzania kama ilivyoainishwa katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba na makubaliano mbalimbali ya kimataifa. Katika jitihada za taifa kupambana na adui ujinga, umaskini na maradhi, uwezo wa wananchi kusoma, kuandika na kuhesabu ni kigezo muhimu sana katika ukombozi binafsi wa kifikra, kijamii na kiuchumi. Hivyo, katika ngazi ya halmashauri, utoaji wa honoraria utazingatia maelekezo yaliyomo katika nyaraka na miongozo ya serikali katika utoaji wa elimu ya watu wazima.

## 4.3 Muundo wa Uendeshaji

Mpango utatumia wataalamu waliopo kwenye mfumo rasmi wa ajira serikalini. Watakaohusishwa katika muundo huu wa uendeshaji ni TEWW, wakuu wa shule, vyuo na taasisi zote za umma, maafisa elimu kata, pamoja na maafisa elimu watu wazima katika halmashauri husika. Uendeshaji wa MECHAVI, utatekelezwa kuanzia ngazi ya kituo hadi taifa. Muundo wa uendeshaji wa mpango huu utakuwa kama ifuatavyo:

### A. Kamati ya Usimamizi ya Kitaifa (KUK)

Kutakuwa na kamati ya usimamizi ngazi ya kitaifa (KUK) ambayo itaundwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST) kwa ajili ya kusimamia shughuli za mpango kwa kiwango cha taifa. Katika kutekeleza majukumu yake, KUK itakuwa na vikao viwili kila mwaka na kwamba katibu wake atakuwa ni TEWW wakati mwenyekiti wake atachaguliwa na katibu mkuu wa WEST. KUK-MECHAVI ambayo itaundwa na Katibu Mkuu wa WEST ikijumuisha wajumbe tofauti kutokana na umuhimu wao kwenye masuala ya uwezeshaji wa elimu kwa walioikosa. Wajumbe wa KUK watachaguliwa kutoka maeneo yafuatayo:

i. Vyuo vikuu: mjumbe mmoja.
ii. NG'Os: mjumbe mmoja.
iii. VETA: mjumbe mmoja.
iv. SIDO: mjumbe mmoja.
v. TET: mjumbe mmoja.
vi. Walimu wa MECHAVI: wajumbe wawili.
vii. NACTE: mjumbe mmoja.
viii. TEWW: mjumbe mmoja.
ix. WEST: wajumbe watatu kutoka Elimu Msingi, Elimu ya Ufundi, na Elimu ya Watu Wazima.
x. TAMISEMI: mjumbe mmoja.
xi. UNICEF: mjumbe mmoja.
xii. ILO: mjumbe mmoja.
xiii. UNESCO: mjumbe mmoja.

## B. Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)

TEWW itaratibu utekelezaji wa shughuli za MECHAVI kwa kufuatilia, kusimamia, na kutathmini utekelezaji wa mpango katika ngazi ya halmashauri na vituo vya mafunzo, kwa kutoa ripoti kwa KUK mara mbili kwa mwaka. Vile vile TEWW itaandaa vikao vya KUK kama itavyohitajika.

Pamoja na hayo, katika ngazi ya Mkoa, TEWW itaratibu shughuli za MECHAVI kupitia Mkufunzi Mkazi wa Mkoa ambaye atawajibika kufanya mambo yafuatayo:

i. Kuunganisha TEWW na wadau wa MECHAVI katika mkoa. Wadau hawa wanajumisha: Halmashauri za wilaya, miji na manispaa, VETA, SIDO, NG'Os, WEOs, Taasisi za kifedha, watu binafsi na ofisi ya elimu mkoa.

ii. Kuratibu utekelezaji wa mpango kwa kushirikiana na afisa elimu watu wazima wa halmashauri husika kupitia afisa elimu msingi.

iii. Kutoa taarifa za MECHAVI makao makuu ya TEWW mara nne kwa mwaka na wakati wowote itakapohitajika.

## C. Afisa Elimu Kata

Afisa Elimu Kata atasimamia na kufuatilia utekelezaji wa mpango. Kutokana na mamlaka yake, yeye ndiye mratibu wa mpango wa MECHAVI katika eneo lake. Atatakiwa kutoa taarifa kwa wadau mbalimbali, kuhamasisha jamii akishirikiana na wenyeviti wa vijiji ili kufanikisha utekelezaji wa mpango.

## D. Mkuu wa Shule/Taasisi

Mkuu wa Shule/Taasisi ndiye msimamizi wa shughuli za MECHAVI katika ngazi ya kituo. Katika kutekeleza majukumu yake atakusanya na kutunza taarifa za mpango kulingana na miongozo itakayotolewa.

## E. Walimu

Walimu wenye umahiri wa kutosha ndio pekee watakaohusishwa katika ufundishaji. Vilevile, walimu hawa wataandaa taarifa za maendeleo ya mpango katika ngazi ya kituo. Mmojawapo wa walimu katika kila kituo atakuwa ni Mratibu wa Mafunzo.

programu hii inasisitiza [illegible]
uendeshaji wake katika maeneo yafuatayo:

i. Kutambua walengwa.

ii. Kuwasajili au kuwaandikisha walengwa katika vituo husika.

iii. Kutoa maeneo ya kufundishia/kujifunzia kama vile majengo, [illegible] kufundishia/kujif[illegible]

karakana au chamb[illegible]

# SURA YA TANO

# USHIRIKISHWAJI NA UBIA

## 5.1 Utangulizi

Ili kufanikisha utekelezaji wa programu hii, ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wakiwemo wazazi, walezi, jamii, sekta ya umma na binafsi ni muhimu. Hivyo, wadau hawa watashirikishwa katika kufanikisha mpango huu.

## 5.2 Ushiriki wa Wazazi, Walezi na Jamii

Malezi na maendeleo ya mtoto huanzia katika ngazi ya familia, ikisaidiana na jamii inayomzunguka. Ushiriki wa wazazi au walezi na jamii kwa ujumla katika kuboresha elimu ni jambo muhimu kwa malezi ya vijana, hususani ushiriki wao katika kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kitaaluma, kijamii na kwa ujumla wake. Hivyo basi, programu hii inasisitiza ushiriki wa wazazi, walezi na jamii kufanikisha uendeshaji wake katika maeneo yafuatayo:

i. Kutambua walengwa.

ii. Kuwasajili au kuwaandikisha walengwa katika vituo husika.

iii. Kutoa maeneo ya kufundishia/kujifunzia kama vile majengo, karakana au shamba darasa.

iv. Kufuatilia maendeleo ya ushiriki wa walengwa katika mchakato mzima wa mafunzo.

## 5.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi

Sekta ya Elimu na Mafunzo ni eneo muhimu la kustawisha ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi. Lengo kuu ni kuongeza uwezo katika kupanua taaluma na huduma mbalimbali katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Serikali imeweka utaratibu wa ubia kati yake na sekta binafsi katika utekelezaji wa programu za elimu. Ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza elimu, utajumuisha mambo mbalimbali yakiwemo:

i. Kuchangia gharama za mafunzo.
ii. Kusaidia walengwa hususani wenye mahitaji maalumu.
iii. Kutoa vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia.
iv. Kujenga, kukarabati na/au kukarafati miundombinu ya kusomea na kujifunzia.

## 5.4 Wadau Wakuu

Wadau wakuu katika mpango huu ni:

i. Wizara mbalimbali (TAMISEMI; Wizara ya Fedha; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto; Wizara ya Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Wizara ya Viwanda na Biashara).
ii. Taasisi za Fedha (VICOBA, BRAC, FINCA, SACCOS, PRIDE, ACCES, POSTA, CRDB, NMB).
iii. Mashirika ya Kimataifa (UNESCO, UNDP, DFID, GIZ, WB, COL, UNICEF, SIDA, GAC, UNFPA, ILO).
iv. Taasisi za Kitaifa za umma (TEA, TBC, NECTA, NACTE, Vyuo vikuu, VETA, TET, SIDO, TLSB, TASAF, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi).
v. Mashirika yasiyo ya serikali (FBOs, CBOs na NGOs). Mashirika haya yanaweza kuanzisha vituo, kuruhusu matumizi ya miundombinu yao kutumiwa kama madarasa, karakana na vituo vya sayansi kimu.
vi. Makampuni ya Umma na Binafsi (makampuni ya simu, vinywaji, migodi, vyombo vya habari, viwanda na wafanyabiashara wa aina zote).

# SURA YA SITA

# KUTHIBITI NA KUKUZA UBORA WA MECHAVI

## 6.1 Utangulizi

Kufanikiwa kwa MECHAVI kutategemea zaidi uangalizi wa karibu na tathmini za mara kwa mara ili kupata ubora uliokusudiwa. MECHAVI itaanzisha njia za kuthibiti ubora ili kuifanya itimize malengo ya uanzishwaji wake.

## 6.2 Mifumo ya Kuthibiti Ubora wa MECHAVI

Kutakuwa na mfumo wa kuthibiti ubora ili kuhakikisha kuwa elimu itolewayo inakidhi viwango vilivyowekwa. Katika kuhakikisha mpango wa MECHAVI unatekelezwa kwa ufanisi, mfumo wa kuthibiti ubora utawahusisha wadau/taasisi mbalimbali. Wadau hao ni:

i. Kamati ya Taifa ya Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule.
ii. Kamati za Kanda za Uthibiti Ubora.
iii. Wakurugenzi wa VETA Kanda.
iv. Meneja wa SIDO mkoa.
v. Mkufunzi Mkazi wa Mkoa wa TEWW.
vi. Afisa Elimu ya Watu Wazima Mkoa.
vii. Afisa Elimu wa Wilaya (Msingi).
viii. Afisa Elimu ya Watu Wazima Wilaya.
ix. Wathibiti ubora wa wilaya.
x. Afisa Elimu Kata.
xi. Wakuu wa Vituo.
xii. Waratibu wa Vituo.

Wadau/taasisi hizo ndizo zitasimamia ubora wa mpango huu hasa katika maeneo ya ujifunzaji (stadi za KKK, Stadi za Maisha, Stadi za Ufundi wa Awali na Ujasiriamali). Hata hivyo, wadau hao watapewa mafunzo maalumu ya utekelezaji wa mpango huu.

### 6.3 Viashiria vya Ubora

Ili kuhakikisha ubora wa elimu itolewayo katika mpango huu, viashiria vifuatavyo vitazingatiwa katika maeneo mbalimbali:

#### 6.3.1 Wawezeshaji / Walimu

Wawezeshaji wa mpango huu watatoka katika taasisi za serikali zilizopo. Wawezeshaji hao wanatakiwa kuwa na umahiri katika fani zao, ujuzi wa stadi za kisomo na stadi za mawasiliano pamoja na kuwa na sifa zinazowawezesha kutoa mafunzo yanayokidhi ubora.

#### 6.3.2 Zana za Kujifunzia na Kufundishia

Katika mpango wa MECHAVI zana mbalimbali za kufundishia na kujifunzia zitaandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya fani husika. Zana hizo zitajumuisha miongozo, vitabu vya kiada na vifaa/zana kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

#### 6.3.3 Kituo cha Kujifunzia

Kituo kitakachoanzishwa kitatakiwa kuwa na vigezo na sifa zitakazowezesha mafunzo kuendeshwa kwa ufanisi. Vigezo hivyo vitazingatia fani zitakazofundishwa katika kituo husika. Vigezo hivyo ni kama vile kufikika kwa urahisi na walengwa wengi na usalama wa kituo.

#### 6.3.4 Viashiria Vingine

Viashiria vingine vitaibuliwa kulingana na mahitaji yatokanayo na taarifa mbalimbali kulingana na wakati husika. Viashiria hivi ni kama maudhui na ubora wa vitabu vya kujifunzia na kufundishia, uwezo wa wanafunzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu, usahihi na ukamilifu wa mafunzo na kiwango cha ushiriki wa wanafunzi darasani.

### 6.4 Mifumo ya Ukusanyaji na Utunzaji wa Takwimu

Uwepo wa mfumo wa ukusanyaji na utunzaji wa takwimu katika mpango wa MECHAVI ni muhimu kwani itasaidia kuelewa mwelekeo mzima wa mpango huu kama vile mchakato mzima wa ujifunzaji na ufundishaji. Takwimu hizo zitahifadhiwa makao makuu ya TEWW katika mfumo wa *Software Learning Management System.* Takwimu hizo zitahusisha maeneo makuu yafuatayo:

i. Taarifa za wanafunzi.
ii. Taarifa za walimu.
iii. Taarifa ya vituo vya kujifunzia.
iv. Taarifa za maendeleo ya wanafunzi.
v. Tathmini ya mtaala.

Ukusanyaji na utunzaji wa takwimu hizi utaanzia ngazi ya kituo ambapo msimamizi mkuu wa kituo atatuma taarifa hizo kwa Mkufunzi Mkazi wa TEWW wa mkoa husika. Mkufunzi Mkazi wa Mkoa atawasilisha taarifa hizo makao makuu ya TEWW ambapo zitahifadhiwa katika mfumo wa utunzaji kumbukumbu wa taasisi kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

## 6.5 Zana za Ufuatiliaji

Ili kuhakikisha zoezi la ufuatiliaji wa kazi mbalimbali katika mpango huu linafanyika kwa ufanisi, zana mbalimbali zitatumika:

i. Taarifa za utekelezaji.
ii. Fomu za mahudhurio na tathmini.
iii. Miongozo ya kufundishia na kujifunzia.
iv. Mpangokazi wa utekelezaji wa mpango wa MECHAVI.

Zoezi hili litafanyika kulingana na miongozo itakayotolewa na pia kutegemeana na mahitaji maalumu ya kituo husika.

## 6.6 Mikakati ya Kukuza Ubora

Ili kuhakikisha kuwa malengo ya mpango huu yanafikiwa katika viwango vilichokusudiwa, mambo yafuatayo yatazingatiwa katika ngazi zifuatazo:

### 6.6.1 Ngazi ya Taifa

Kamati ya Usimamizi ya Taifa ya mpango huu itakutana mara mbili kwa mwaka ili kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji za MECHAVI na hatimaye kutoa ushauri, maelekezo na miongozo kwa ajili ya maboresho.

### 6.5.2 Ngazi ya Mkoa

Mkufunzi mkazi wa TEWW, Mthibiti Ubora Kanda na Mratibu wa Elimu ya Watu Wazima Mkoa watakutana kila robo mwaka ili kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa mpango kutoka katika Halmashauri za Wilaya na vituo hatimaye kutoa ushauri, maelekezo na miongozo kwa ajili ya maboresho.

Kamati hii pia itavitembelea vituo angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu ili kujionea utendaji kazi katika vituo vinavyotekeleza mpango wa MECHAVI.

### 6.6.3 Ngazi ya Wilaya

Maafisa Elimu Watu Wazima, Maafisa Elimu Kata, Wakuu wa Vituo na Waratibu wa Vituo watakutana mara moja kwa mwezi kujadili utekelezaji wa MECHAVI katika ngazi ya kata. Wanakamati hao watashauri vema jinsi MECHAVI inavyotolewa na inavyotakiwa kuwa kwa kuandika ripoti na kuituma makao makuu ya mkoa.

### 6.6.4 Ngazi ya Kata

Maafisa Elimu Kata, Wakuu wa Vituo na Waratibu wa Vituo. Hawa watakutana mara moja kwa mwezi kutathmini utekelezaji wa MECHAVI katika Kata na kushauri kulingana na yaliyojiri. Pia wataandaa taarifa ya utekelezaji na kuituma makao makuu ya wilaya.

### 6.6.5 Ngazi ya Kituo

Katika ngazi ya kituo, kutakuwa na Mkuu wa Kituo, Mratibu wa Kituo na Walimu/wawezeshaji ambao watasimamia na kutekeleza mtaala huu. Hawa watakuwa wanaandaa ripoti za kila mwezi.

Wawezeshaji watakuwa na jukumu la kufundisha kulingana na fani zao kwa kufuata miongozo iliyoandaliwa. Pia wataandaa taarifa ya tathmini na kuiwasilisha kwa Mratibu wa Kituo. Aidha, wawezeshaji watahakikisha kuwa wanafundisha masomo yao kwa weledi mkubwa.

Kituo kitahakikisha kuwa watendaji wote katika kituo wanapatikana kwa kufuata vigezo vilivyoainishwa katika mtaala huu. Watendaji hao watapatiwa mafunzo ya awali na baadaye mafunzo ya mara kwa mara kutokana na mahitaji ili kuhakikisha kuwa mtaala huu unatekelezwa kwa mujibu wa matokeo yaliyokusudiwa.

## 6.7 Tathmini ya Matokeo

Tathmini ya matokeo itabaini mafanikio ya utekelezaji wa MECHAVI. Aidha, kutokana na mabadiliko chanya ya mpango huu, yatajionesha kupitia kwa walengwa. Kwa mfano, kujua kusoma, kuandika, kuhesabu na uwezo wa kuchangamana na watu wengine katika jamii, uwezo wa kumudu ujuzi mpya katika maisha, matumizi ya teknolojia na biashara. Vilevile tathmini itaonesha mabadiliko chanya ya washiriki na jamii katika kumudu mazingira yao kama matokeo ya utekelezaji wa MECHAVI.

## 6.8 Hitimisho

Kila ngazi itawajibika kubaini changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mpango huu na kuzitatua. Hatimaye changamoto zilizo nje ya uwezo wao wataziwasilisha katika ngazi ya juu kwa ajili ya kupatiwa majibu sitahiki.

**Printed By:** Institute of Adult Education
S.L.P 20679, Dar es Salaam, Tanzania
Tel:+255 22 2150838, Fax: +255 22 2150836
Website:www.iae.tz Email:info@iae.ac.tz